



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA



Kumb. Na.MDC/A.70/73/VOL.VI/145

24/10/2024

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
Kiwanja Na.9A & B,
Mtaa wa Shaaban Robert,
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

YAH: UTAMBULISHO WA HUADA LIMITED,MWEKEZAJI WA VIWANDA
KATIKA WILAYA YA MKURANGA.

Rejea mada tajwa ya barua hapo juu.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) imepokea maombi kutoka kwa kampuni ya **HUADA LIMITED**,kupitia barua yao ya tarehe 24/10/2024 ikiomba kutambulishwa katika Taasisi yako. **HUADA LIMITED** ni kampuni ya kigeni,ambayo imesajiliwa hapa nchini na Wakala wa usajili wa biashara na leseni(Brela), kwa hati ya usajili (Certificate of Incorporation of a Company), Na. 164489698 ya tarehe 21 Machi,2023.

Kwa barua hii tunathibitisha kwako,kwamba kampuni hii ina dhamira ya dhati katika kufanya uwekezaji wa Viwanda katika Wilaya ya Mkuranga. Katika kuthibitisha hilo Kampuni hii tayari imenunua ardhi yenye ukubwa wa mita za mraba 30,572 ,kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Ardhi hii imepangwa na kwa kuandaliwa Mchoro wa Mipangomiji,uliosajiliwa kwa TP Na. 19/MK/240/062023, na kupimwa kupitia Ramani ya Upimaji iliyosajiliwa tarehe 24/08/2023 kwa Na. 183274 (Registered Plan Na. 183274).

HUADA LIMITED wameomba kibali cha ujenzi wa uzio (Fence) na Majengo ya kiwanda,ambapo wamepatiwa kibali cha Ujenzi (Building permit) Na.0271 kilichotolewa mnamo tarehe 16,Mei,2023. Wawekezaji hawa wameshaanza ujenzi,ambapo hadi sasa wameshajenga Uzio (Fence),Jengo la Wafanyakazi na Kibanda cha Mlinzi.

Aidha,napenda kukuthibitishia kwamba,tangu kuingia kwake hapa Wilayani Mkuranga **HUADA LIMITED** wamelipa kodi na ada zote inavyostahili,na kwamba wanatoa ushirikiano mzuri kwa serikali na jamii ya wananchi wa Mkuranga kwa ujumla.

Pamoja na barua hii tumeambatanisha nyaraka zifuatazo;

- i. Kivuli cha Memorandum and Articles of Association ya **HUADA LIMITED**.
- ii. Kivuli cha hati ya usajili wa Kampuni(Certificate of Incorporation of a company).

Director Office, Mkuranga, S.L.P 10, Mkuranga District Council, Phone: 023-2110038, Faxi: 023-2110038.
Email: ded@mkurangadc.go.tz, Tovuti: www.mkurangadc.go.tz

- iii. Kivuli cha Mkataba wa ununuzi wa Ardhi.
- iv. Kivuli cha Muhtasari wa kikao cha Halmashauri ya Kijiji cha Mkuranga.
- v. Kivuli cha Ramani ya Mipango miji.
- vi. Kivuli cha Ramani ya upimaji (Registered Plan No.183274).
- vii. Kibali cha Ujenzi (Building Permit No. 0271).

Nakutakia kazi njema.


.....

Wilbert J. Mduma

Kny; Mkurugenzi Mtendaji (W)

MKURANGA



Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W) - Kwa taarifa

S.L.P 10

MKURANGA.

Mkurugenzi Mtendaji - taarifa

HUADA LIMITED

S.L.P 161

MKURANGA.